

Kufuatia kuungua kwa mara ya pili kwa soko kuu la kayanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, Ofisi ya Mkuu wa mkoa Kagera imeiagiza Halmashauri hiyo kuunda timu mara moja na kuanza uchunguzi wa chanzo cha moto huo katika soko hilo, ambalo kwa mara ya kwanza liliungua tarehe 11 Machi, 2016.

Sehemu ya soko kuu la Kayanga imeungua usiku wa kuamkia tarehe 7 Januari, 2016, saa 9:00 usiku, ambapo vibanda 52 vilivyojengwa kwa mbao na meza 24 za wafanyabashara wadogowadogo wa nafaka, matunda na mbogamboga vimeteketee kwa moto pamoja na mali za wamachinga waliokuwa wanapanga chini wapatao 33 nao mali zao zimeteketee kwa moto.

Akiongea mara baada ya kukagua athari za janga la moto katika soko hilo Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera Kamishna Diwani Athumani, leo tarehe 7 Januari, 2017, amebainisha kuwa tayari Halmashauri ya wilaya hiyo imeshatekeleza maelekezo yao ya kuunda timu ya uchunguzi ambayo inanza kutekeleza majukumu yake kesho, tarehe 8 Januari, kwa muda wa siku nne.

“Tumeunda timu tujue kwa nini hili soko linakuwa na majanga ya moto ya mara kwa mara, nawaomba wananchi wote wa Kayanga towneni ushirikiano wa kutosha kwa timu hii na yeyote mwenye taarifa ya chanzo cha moto awasilishe taarifa zake kwenye kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hii” Alisisitiza Athumani.

Aidha, Athumani alifafanua kuwa yeyeyote atakaye bainika kuwa ndo chanzo cha kusababisha majanga ya moto kutokea mara kwa mara katika soko hilo hatua stahiki zitachukuliwa kwa kuwa kuungua kwa soko hilo kumesababisha hasara kubwa kwa wafanyabiashara wa soko hilo.

Akiongea wakati wa ziara hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Adeodata Augustine, amefafanua kuwa thamani ya awali ya mali iliyoteketee inakisiwa kuwa Tsh, 80,000,000/= (mazao ya nafaka, mbogamboga, matunda pamoja na nguo na bidhaa za dukani), na thamani ya vibanda ni Tsh, 52,000,000/= na meza ni 9,600, 000/=.

“Chanzo cha moto hadi sasa hakijajulikana na kikosi cha zimamoto kwa kushirikiana na Polisi

na TANESCO wanaendelea na uchunguzi, taarifa hii ni ya awali tutapata taarifa kamili ya thamani ya mali na chanzo cha janga la moto baada ya timu kukamilisha kazi kwa muda uliopangwa” alisema Adeodata.

Naye mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Soko kuu la Kayanga, Wilton William, aliishukuru halmashauri hiyo kwa juhudi walizo zifanya za kuzima moto huo pamoja na hatua walizozichukua za kuchunguza chanzo cha moto huo ambao umeunguza soko hilo kwa mara ya pili mfululizo.

Soko la Kayanga lina jumla ya vibanda 257, ambapo vibanda 122 vimejengwa kwa matofali, na vibanda 135 vimejengwa kwa mbao. Katika tukio la janga la moto la mwaka jana vibanda 117 ikiwa ni vibanda 83 vya mbao na 34 vya tofali viliteketea kwa moto.

Mwisho.